JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**Anuaniyasimu "ELIMU"**
**Simu: 026 296 35 33**
**Baruapepe:info@moe.go.tz**
**Tovuti: www.moe.go.tz**
**Unapojibu tafadhali taja:**

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
**40479 DODOMA**

**Kumb.Na. CA.229/238/01/14**

**30 Juni, 2022**

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P. 2662,
**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P. 1454,
**DAR ES SAALAM.**

Katibu Mtendaji,
Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
**DAR ES SAALAM.**

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Inventors in Education (TAPIE),
S.L.P. 13346,
**DAR ES SAALAM.**

Mwenyekiti
Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA),
S.L.P. 8581,
**DAR ES SAALAM.**

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S.L.P. 13547,
**DAR ES SALAAM**.

**WARAKA WA ELIMU NA. 4 WA MWAKA 2022 KUHUSU UIMARISHAJI WA MAZINGIRA YA SHULE KUWA SALAMA NA WEZESHI KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI**

Mazingira salama na wezeshi ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji ili kukuza uwezo wa mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, kujiamini na kushiriki katika shughuli mbalimbali shuleni. Mazingira salama na wezeshi shuleni ni jumla ya mambo yote yanayompa mwanafunzi fursa anuai katika kujifunza, kucheza na kuchunguza kwa uhuru bila hofu au woga wa aina yoyote. Mazingira haya humpa mwanafunzi nafasi ya kukua vema kimwili, kiakili, kijamii na kimaisha katika kujifunza.

2. Mazingira haya hutoa fursa kwa wanafunzi kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji, kujiamini, kuwajibika, kutafakari na kuchambua masuala mbalimbali na kutatua changamoto kulingana na mazingira. Wanafunzi wanapokuwa katika mazingira salama na wezeshi ni wazi kuwa watajihisi kuwa wako salama hivyo kuwa rahisi kwao kuwa watulivu, wabunifu na wadadisi. Waraka huu unalenga kuimarisha mazingira ya shule kuwa salama na wezeshi ili kuboresha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

3. **Majukumu ya Wadau Mbalimbali**

Jukumu la kuimarisha mazingira ya shule kuwa salama na wezeshi ni suala la wadau wote wa elimu. Katika kutimiza jukumu hili wadau watatekeleza majukumu yafuatayo:

**i) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST)**

a) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uimarishaji wa mazingira ya shule kuwa salama na wezeshi katika kuleta ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji;

b) Kutoa taarifa ya ufuatiliaji na tathmini kwa wadau mbalimbali wa elimu;

c) Kutoa mafunzo ya uimarishaji mazingira ya shule kuwa salama na wezeshi katika ufundishaji na ujifunzaji;

d) Kufanya tafiti kuhusu usalama wa wanafunzi shuleni ili kubaini na kutatua changamoto zinazoathiri usalama wa watoto shuleni;

e) Kutoa vifaa vya Elimu kwa wanafunzi wote ikiwemo vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;
f) Kuhakikisha uwepo wa miundombinu fikivu na rafiki kwa wanafunzi wote;
g) Kuratibu na kushirikiana na wadau wa Elimu katika kuimarisha mazingira salama na wezeshi shuleni; na
h) Kuandaa na kupitia miongozo na nyaraka mbalimbali zinazohusu usalama wa mazingira ya shule ili kuendana na mahitaji ya wakati husika.

**ii) Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)**

a) Kutoa taarifa mbalimbali kwa Wizara ya Elimu kuhusu utekelezaji wa uimarishaji wa mazingira ya shule;
b) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uimarishaji wa mazingira wezeshi mara kwa mara;
c) Kusimamia ngazi ya Mikoa na Halmashauri katika kuimarisha mazingira salama na wezeshi katika ufundishaji na ujifunzaji;
d) Kutekeleza mipango na mikakati ya uimarishaji wa mazingira ya shule salama na wezeshi; na
e) Kuimarisha miundombinu kuwa fikivu, salama na wezeshi.

**iii) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa**

a) Kusimamia Halmashauri zote katika uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni;
b) Kuboresha miundombinu katika Halmashauri kuwa fikivu,salama na wezeshi shuleni;
c) Kushikirikiana na wadau katika ngazi ya mkoa kuimarisha mazingira ya shule kuwa salama na wezeshi;
d) Kuandaa Taarifa ya mkoa inayohusu utekelezaji wa uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni; na
e) Kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ya uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni kulingana na mazingira.

iv) **Halmashauri**

a) Kutekeleza malengo na mikakati ya uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi katika ufundishaji na ujifunzaji;

b) Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya Halmashauri ya utekelezaji wa uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni;

c) Kushirikiana na wadau katika ngazi ya Halmashauri kuboresha mazingira salama na wezeshi shuleni;

d) Kuandaa Taarifa ya Halmashauri ya utekelezaji wa uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni;

e) Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

f) Kushirikiana na walimu na jamii ili kubaini changamoto zinazokabili shule katika uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi na kutafuta ufumbuzi;

g) Kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata vifaa vya elimu na saidizi; na

h) Kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ya uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni kulingana na mazingira.

v) **Bodi ya Shule**

a) Kushirikiana na Uongozi wa Shule, wazazi/walezi katika kubaini changamoto zinazowakabili wanafunzi na kufanya maamuzi sahihi yahusuyo usalama wa mwanafunzi;

b) Kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu viashiria vinavyoweza kuhatarisha uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni; na

c) Kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ya uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni kulingana na mazingira.

vi) **Mkuu wa Shule**

a) Kusimamia utekelezaji wa miongozo na nyaraka mbalimbali zinazohusu usalama wa mwanafunzi awapo shuleni;

b) Kusimamia ufundishaji, ujifunzaji na nidhamu ya walimu na wanafunzi ndani na nje ya shule;

c) Kushirikiana na Bodi ya Shule, walimu, wazazi/walezi, wanafunzi na jamii katika kubaini na kutatua changamoto mbalimbali za kiusalama zinazowakabili wanafunzi;

d) Kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ya uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni kulingana na mazingira; na

e) Kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu viashiria na vinavyoweza kuhatarisha uimarishaji wa mazingira salama na wezeshi shuleni.

**vii) Mwalimu**

a) Kusimamia nidhamu shuleni;

b) Kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi;

c) Kuhakikisha mazingira ya shule ni safi, salama na fikivu kulingana na mahitaji mbalimbali ya wanafunzi wote.

d) Kushirikiana na wazazi katika kubaini na kutatua changamoto mbalimbali zinazoathiri uasalama wa wanafunzi ndani na nje ya shule;

e) Kushirikiana na wazazi/walezi kutoa taarifa ya viashiria, matendo yanavyoathiri usalama wa wanafunzi ndani na nje ya shule;

**viii) Mwanafunzi**

a) Kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wasio walimu, wazazi, walezi na watu wazima wakati wote awapo shuleni na nje ya shule;

b) Kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule;

c) Kutoshiriki katika vitendo vinavyoathiri usalama wake na wa wanafunzi wengine;

d) Kutunza na kulinda samani na mazingira ya shule; na

e) Kutoa taarifa kwa walimu/wazazi/walezi wanapokabiliana na viashiria na matendo yanayoathiri usalama binafsi na wanafunzi wenzake.

**ix) Wazazi/Walezi**

a) Kusimamia nidhamu ya watoto wao wawapo nyumbani;

b) Kutoa ushauri kwa watoto wao juu ya namna bora ya kujilinda na kulinda usalama wa wenzao;

c) Kushirikiana na walimu katika kubaini na kutatua changamoto mbalimbali wanazokutana nazo wanafunzi nje ya shule; na

d) Kushirikiana na walimu kutoa taarifa za matendo yanayoathilri usalama wa watoto.

**Waraka huu unaanza kutumika tarehe 01 Julai, 2022**

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

KAMISHNA WA ELIMU

**Nakala**: Wathibiti Ubora Wakuu wa Shule Kanda;
Wathibiti Ubora Wakuu wa Shule Wilaya.

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

*Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*